

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA



**MKUTANO MAALUM WA BARAZA LA MADIWANI (BAJETI)
UTAFANYIKA TAREHE 17 FEBRUARI, 2022**

**MAHALI: UKUMBI MKUBWA WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA
JIJI LA DODOMA**

MUDA: SAA 4:00 ASUBUHI

Mkurugenzi,
Halmashauri ya Jiji,
S.L.P 1249,
DODOMA.

Simu: +255026-2354817
Nukushi: +25526-2321550
Baruaapepe: cd@dodomacc.go.tz
Tovuti: www.dodomacc.go.tz
Instagram: dodomajiji_tz
Facebook: Dodoma Jiji
Youtube: Dodoma City TV



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. HJD/C.40/7/13

10 Februari, 2022

Mstahiki Meya,
Mh. Naibu Meya,
Wah. Wajumbe wote,
Baraza la Madiwani,
Halmashauri ya Jiji,
DODOMA.

**YAH: WITO WA KUHUDHURIA MKUTANO MAALUM WA BARAZA LA MADIWANI
(BAJETI) UTAKAOFANYIKA TAREHE 17.02.2022**

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu.

Napenda kuwajulisha kuwa, Mkutano Maalum wa Baraza la Madiwani kwa ajili ya kupitia Mapitio ya Bajeti ya mwaka 2021/2022 pamoja na Mpango wa Makisio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2022/2023, utafanyika tarehe 17.02.2022 kuanzia saa 4:00 asubuhi katika Ukumbi Mkubwa wa Mikutano wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Agenda zitakazo jadiliwa:

1. Kufungua Mkutano.
2. Kupitia mapitio ya Bajeti ya mwaka 2021/2022 pamoja na Mpango wa Makisio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2022/2023.
3. Kufunga Mkutano.

Joseph C. Mafuru

**MKURUGENZI WA JIJI
DODOMA**

YALIYOMO

MAELEZO	UKURASA
Utangulizi	1-5
Mapitio ya Bajeti 2020/21 na 2021/22	5-12
Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/23	12-22
	23
MATUMIZI MENGINEYO RUZUKU(OC)	
Afya OC	24-28
Elimu Sekondari	29-30
Elimu Msingi	31
Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika	32-33
Mifugo na Uvuvi	34
Ujenzi	35
MATUMIZI YA KAWAIDA MAPATO YA NDANI	36
Utarwala	37-43
Ardhi Mipango Miji na Maliasili	44-46
Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji	47-51
Mifugo na Uvuvi	52-56
Elimu Msingi	57-60
Maendeleo ya Jamii na Vijana	61-70
Mazingira na Udhibiti taka ngumu	71-73
Ujenzi	74-76
Afya	77-91
Afya CHF	92-93
Afya NHIF	94-95
Afya Papo kwa Papo (USERFEE)	96
Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika	97-102
Fedha na Biashara	103-107
Sheria	108-111
Manunuzi	112-114
Nyuki	115-116
Ukaguzi wa Ndani	117-120
TEHAMA	121-123
Uchaguzi	124-126
Elimu Sekondari	127-129
MIRADI YA MAENDELEO MAPATO YA NDANI	130
Ardhi Mipango Miji na Maliasili	131-134
Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji	135-137
Mifugo na Uvuvi	138
Maendeleo ya Jamii na Vijana	139

MAELEZO	UKURASA
Elimu Msingi	140-141
Mazingira na Udhibiti taka ngumu	142
Ujenzi	143-144
Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika	145-146
Fedha na Biashara	147
Tehama	148-149
Utawala	150-151
Elimu Sekondari	152-154
Afya	155-156
MIRADI YA MAENDELEO SERIKALI KUU	157
Mipango, Takwimu na Ufutiliaji	158
Elimu Msingi	159
Elimu Sekondari	160-163
Elimu Msingi	164-166
MIRADI YA MAENDELEO WAFADHILI	167
Elimu Msingi – EP4R	168-169
Afya HSBF	170-177
Maendeleo ya Jamii na Vijana (TASAF)	178

HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

MHESHIMIWA MWENYEKITI,
BARAZA LA MADIWANI,
HALMASHAURI YA JIJI,
DODOMA.

MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

Utangulizi

Katika kuandaa Mpango na Bajeti ya mwaka 2022/23, Halmashauri ya Jiji la Dodoma imetumia miongozo mbalimbali katika kufanikisha kazi hii, Aidha utaratibu wa kuandaa mpango shirikishi wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O & OD) ulizingatiwa katika kuibua miradi inayotokana na jamii katika ngazi ya Kata na Mitaa. Miradi ambayo itatekelezwa katika ngazi ya Kata na Mitaa imetokana na vipaumbele vya jamii kwa mfumo wa O & OD.

Mpango na Bajeti ya mwaka 2022/23 imezingatia mambo yafuatayo:-

I. Miongozo mbalimbali.

1. Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020-2025)
2. Michango/Maoni kutoka katika Vikao vya Kamati za kudumu za Halmashauri (Uchumi, Mpango Miji na Fedha) vitakavyojadili Bajeti hii.
3. Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti 2022/23.
4. Mpango Mkakati wa Halmashauri ya Jiji (Strategic Plan) kwa mwaka 2021/22 – 2025/26.
5. Agizo/Amri namba 15,16,17 na 19 Kanuni ya fedha za Serikali za Mitaa 2009 (The Local Authority financial memorandum) vimezingatiwa katika kuandaa makisio haya
6. Agizo 16(2) ambalo linataka jumla ya makisio ya matumizi ya kawaida kulingana na Jumla ya makisio ya mapato (MATUMIZI = MAPATO) limezingatiwa.
7. Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.
8. Mpango wa Maendeleo wa miaka 5 (2021/22 – 2025/26)

9. Malengo endelevu ya maendeleo (SDG) n.k.

II. Vipaumbele vya Bajeti ya 2022/23

Mwelekeo wa Bajeti ya Halmashauri ya Jiji kwa mwaka wa fedha 2022/23

Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa mwaka wa fedha 2022/23 imejipanga kuelekeza nguvu zake katika maeneo mbalimbali kutokana na mwongozo wa Bajeti na Vipaumbele vya Halmashauri kama ifuatavyo:-

- Kuweka mazingira wezeshi yatakayosababisha kuinua na kukuza uchumi wa Halmashauri na kuinua kipato cha mtu mmoja mmoja katika Jiji la Dodoma kwa kuwekeza katika miundombinu ya uchumi na kutoa mikopo kwa Wanawake, Vijana na Walemavu.
- Fedha zitakazotengwa kwa ajili ya mikopo ya Wanawake, Vijana na Walemavu 60% ya kiasi hicho kitaelekezwa kwenye miradi yenye tija itakayozalisha ajira.
- Kuratibu na kusimamia ufanikishaji wa zoezi la SENSA ya Watu na makazi ya mwaka 2022.
- Kufungua akaunti kwa ajili ya marejesho ya 10% ya Wanawake , Vijana na Walemavu. Pia Marejesho hayo ya mikopo ya 10% yanayotarajiwa kurejeshwa na vikundi vilivyokopeshwa yataingizwa kwenye mpango na bajeti wa mwaka wa fedha 2022/23.
- Mapato yatakayopokelewa kama michango na kutoka kwa wadau wa maendeleo yatajumuishwa kwenye bajeti kwa kuzingatia Sheria kanuni na taratibu zilizopo, Aidha fedha hizo zitatumika kutekeleza miradi yeneye tija ambayo itaanizishwa na kuhakikisha inakamilika katika mwaka wa fedha husika badala ya kuanzisha miradi na kuacha viporo.
- Kutekeleza mwongozo wa OR – TAMISEMI wa utoaji vibali vya ujenzi na usimamizi wa ujenzi wa majengo kwenye Halmashauri uliotolewa Machi, 2018.
- Kuwasilisha kwa Katibu Tawala Mkoa ahadi za fedha za miradi inayopendekezwa kutekelezwa na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO's) na wadau wengine wa maendeleo ili zijimuishwe kwenye Mpango na Bajeti ya Halmashauri.

- Kuboresha miundombinu na utoaji wa huduma bora za afya, elimu na maji kwa jamii. (ujenzi wa madarasa, vituo vya afya, maji na Ufunguzi wa barabara.)
- Kupanga, kupima ardhi na kusimamia uendelezaji na ustawishaji wa mji wa Dodoma ili kuwa na hadhi ya Makao makuu ya Nchi (kupima, kufungua barabara n.k)
- Kuandaa maandiko ambayo yatatumiwa kutafuta fedha kwa ajili ya utaratibu mpya wa ugharamiaji mbadala wa miradi ya maendeleo kwa kuzingatia mwongozo wa Kitaifa wa uandaaji wa miradi uliotolewa na OR – TAMISEMI kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la maendeleo na mitaji (United Nations Capital Development Fund – UNCDF).
- Kutekeleza Miradi kwa kutumia fedha za ndani hasa miradi ya kimkakati ili kupata wawekezaji wakubwa.
- Kuendelea na ujenzi wa mradi wa uwekezaji awamu ya pili mradi wa Government City Complex (kwa kuingia ubia na Taasisi mbalimbali/ Kuomba fedha kutoka serikali kuu).
- Kutangaza miradi yetu iliyosanifiwa ndani na nje ya nchi ili kupata wawekezaji kwa njia za ubia
- Kubuni vyanzo vipya vya kuongeza mapato ya Halmashauri
- Kuweka mikakati ya kuongeza mapato.
- Kubuni mikakati ya kuinua kiwango cha ufaulu kwa shule za Msingi na Sekondari
- Kumalizia ujenzi wa miradi viporo.
- Kuendelea kutatua tatizo la madawati kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kwa kutenga Bajeti maalumu ya utengenezaji wa madawati.
- Kushawishi uwekezaji mkubwa kwenye uendelezaji wa mifugo na uvuvi (ushiriki wa sekta binafsi) na kuboresha masoko ya Mifugo/Uvuvi na bidhaa zake.
- Kuendelea kuhamasisha kilimo cha mazao yanayostahimili ukame ili kuwa na uhakika wa chakula.
- Kuboresha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji ili kuendeleza kilimo cha umwagiliaji.

- Kuhamasisha uundwaji wa vikundi, kuvijengea uwezo na kuwawezesha kiuchumi vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.
- Kutoa elimu ya kujikinga dhidi ya maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI na kuongeza vita ya unyanyapaa dhidi ya wagonjwa wa UKIMWI
- Kuendelea na ujenzi wa kituo cha wajasiriamali eneo la Nzuguni.
- Kutoa elimu ya mikopo na ujasiriamali kwa vikundi vya wanawake vijana na watu wenye ulemavu na kutoa elimu ya stadi za maisha kwa Vijana.
- Kuzijengea uwezo Kamati za kupinga ukatili dhidi ya Wanawake na watoto ngazi ya Wilaya na Kata (MTAKUWWA) pamoja na kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia kwa jamii.
- Kuendelea kutatua migogoro ya ardhi katika Jiji la Dodoma.
- Kusimamia kwa ufanisi ujenzi wa miundombinu katika taasisi za serikali na ujenzi wa miradi ya kimkakati.
- Kuendelea kusimamia na kuhakikisha usafi wa mji ili kuupa hadhi ya Makao makuu ya nchi.
- Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.
- Ujenzi wa Shule ya English Medium
- Kuwezesha mazingira bora kwa Watumishi wa pembezoni.

III. MAENEO YATAKAYOPEWA UMUHIMU KATIKA BAJETI 2022/23

A. Miradi ya Maendeleo.

- Kukamilisha miradi inayoendelea kutekelezwa (Viporo)
- Kuchangia nguvu za wananchi inapobidi .
- Kujenga Miradi ya maendeleo inayoleta tija.
- Kuimarisha sekta ya Elimu, Afya.
- Kuimarisha utoaji wa huduma katika maeneo ya pembezoni.

B. Upande wa watumishi na ofisi.

- Stahiki za watumishi
- Mafuta
- Matengenezo ya magari/vipuri
- Bima ya magari

- Uhamisho
- Matibabu
- Vifaa vya ofisi(vitendea kazi)
- Kompyuta
- Likizo
- Gharama za mazishi
- Posho ya kujikimu kwa watumishi wapya (subsistence allowances)
- Ununuzi wa Fanicha za ofisi .
- Kodi kwa Watumishi katika mifuko ya hifadhi ya Jamii (PSSF)

1.1 MAPITIO YA BAJETI YA MWAKA 2020/21

Katika mwaka wa fedha 2020/21, Halmashauri iliidhinishiwa kukusanya na kutumia jumla ya Shilingi **115,929,803,387** kama ifuatavyo:-

1. VYANZO VYA HALMASHAURI	-	TZS.	47,104,504,276
2. MISHAHARA (PE)	-	TZS	62,320,204,498
3. MATUMIZI MENGINEYO (OC)	-	TZS.	3,783,624,000
4. MIRADI YA MAENDELEO	-	TZS	2,721,470,613
JUMLA	-	TZS	115,929,803,387

1.1.1 MAPITIO YA MAPATO/MAPOKEZI:

Mwaka 2020/21 Halmashauri ya Jiji la Dodoma ilikadiria kukusanya na kutumia jumla ya Shilingi **115,929,803,387** kutoka katika vyanzo mbali mbali. Hadi kufikia tarehe 30/06/2021, Makusanyo/Mapokezi halisi yalikuwa jumla ya Shilingi **93,312,088,948** sawa na asilimia **80%** ya makisio ya mwaka 2020/2021.

Muhtasari wa makusanyo /mapokezi hayo ni kama ifuatavyo:-

NA	CHANZO CHA MAPATO	MAKISIO YA MWAKA 2020/21 (TZS)	MAPATO HADI JUNI 2021 (TZS)	ASILIMIA YA MAKUSANYO/MAPOKEZI (TZS)
1.	VYANZO VYA HALMASHAURI	47,104,504,276	37,486,779,806	80%
2.	MISHAHARA (PE)	62,320,204,498	47,307,452,382	76%
3.	MATUMIZI MENGINEYO (OC)	3,783,624,000	2,665,816,935	70%
4.	MIRADI YA MAENDELEO (RUZUKU)	2,721,470,613	2,095,424,789	77%
	JUMLA	115,929,803,387	89,555,473,912	77%

NB: Mishahara ilitolewa pungufu kwa sababu Jiji ilikasimia kuajiri Watumishi wapya na kupandisha vyeo lakini kibali cha ajira hakikutolewa na vyeo kutokupandishwa kama ilivyotarajiwa.

1.1.2 MATUMIZI

Mwaka 2020/2021, Halmashauri ya Jiji la Dodoma ilikadiria kutumia jumla ya Shilingi **115,929,803,387** kutokana na vyanzo mbali mbali vya mapato. Hadi kufikia tarehe 30/06/2021, Matumizi halisi yalikuwa jumla ya Shilingi **88,181,690,455** sawa na asilimia **76** ya makisio ya mwaka 2020/21.

Muhtasari wa Matumizi hadi kufikia tarehe 30/06/2020 hayo ni kama ifuatavyo:-

NA	CHANZO CHA MATUMIZI	MAKISIO YA MWAKA 2019/2020 (TZS)	MATUMIZI HADI JUNI 2020 (TZS)	ASILIMIA YA MATUMIZI (TZS)
1.	MATUMIZI YATOKANAYO NA MAPATO YA NDANI	47,104,504,276	37,486,779,806	80%
2.	MATUMIZI YA RUZUKU YA MISHAHARA (PE)	62,320,204,498	47,307,452,382	76%
3.	RUZUKU YA MATUMIZI MENGINEYO (OC)	3,783,624,000	1,611,389,520	43%
4.	MIRADI YA MAENDELEO	2,721,470,613	1,776,068,747	65%
	JUMLA	115,929,803,387	88,181,690,455	76%

1.2 MAPITIO YA BAJETI YA MWAKA 2021/22 HADI DESEMBA 2021
 Katika mwaka wa fedha 2021/22, Halmashauri iliidhinishiwa kukusanya na kutumia jumla ya Tshs **127,000,210,329** kama ifuatavyo:-

1. VYANZO VYA HALMASHAURI	-	TZS.	50,116,465,099
2. MISHAHARA (PE)	-	TZS.	62,320,204,498
3. MATUMIZI MENGINEYO (OC)	-	TZS.	1,422,279,200
4. MIRADI YA MAENDELEO	-	TZS.	13,141,261,532
JUMLA			TZS. 127,000,210,329

1.2.1 MAPITIO YA MAPATO/MAPOKEZI:

Mwaka 2021/22 Halmashauri ya Jiji la Dodoma ilikadirira kukusanya/kupokea jumla ya shilingi **127,000,210,329** kutoka katika vyanzo mbali mbali. Hadi kufikia tarehe 31/12/2021, (Julai – Desemba) Makusanyo/Mapokezi halisi yalikuwa jumla ya Tzs. **58,639,176,284** sawa na asilimia **46%** ya makisio ya mwaka 2021/22.

Muhtasari wa makusanyo /mapokezi hayo ni kama ifuatavyo:-

NA	CHANZO CHA MAPATO	BAJETI 2020/21 (TZS)	MAPATO HADI DISEMBA 2021 (TZS)	% YA MAKUSANYO /MAPOKEZI (TZS)
1.	VYANZO VYA HALMASHAURI	50,116,465,099.00	25,699,533,045	51.3%
2.	RUZUKU YA MISHAHARA (PE)	62,320,204,498.00	25,665,165,221	41.2%
3.	MATUMIZI MENGINEYO (OC)	1,422,279,200	848,117,460	59.6%
4	RUZUKU YA MIRADI YA MAENDELEO	13,141,261,532	6,426,360,558	49%
	JUMLA	127,000,210,329	58,639,176,284	46%

N.B Katika mwaka wa fedha 2021/22 tulipokea fedha nje ya Bajeti kiasi cha shilingi **2,963,385,250** hivyo kufanya jumla ya mapato kuwa shilingi **60,993,827,534.00** sawa na asilimia **48** ya mapokezi ya fedha kwa mwaka 2021/22

**1.2.2 MATUMIZI BAJETI YA MWAKA 2021/22 HADI TAREHE 30 DISEMBA,
2020**

Mwaka 2021/2022, Halmashauri ya Jiji la Dodoma ilikadiria kutumia jumla ya Tzs **127,946,202,056** kutokana na vyanzo mbali mbali vya mapato. Hadi kufikia tarehe 31/12/2021, (Julai - Disemba) Matumizi halisi yamefikia jumla ya TZS **45,149,616,414** sawa na asilimia **35.6** ya makisio ya mwaka 2021/22.

Muhtasari wa Matumizi hadi kufikia tarehe 30/12/2021 ni kama ifuatavyo:-

NA	CHANZO MATUMIZI	CHA	MAKISIO MWAKA 2020/2021 (Tzs)	YA	MATUMIZI HADI DESEMBA 2021 (Tzs)	ASILIMIA YA MATUMIZI (Tzs)
1.	MATUMIZI YATOKANAYO NA MAPATO YA NDANI	NA	50,116,465,099		17,516,618,415	35.8
2.	MATUMIZI YA RUZUKU YA MISHAHARA (PE)		62,320,204,498.00		25,665,165,221	41.2
3.	RUZUKU YA MATUMIZI MENGINEYO (OC)		1,422,279,200		863,989,329	60.7
4	MATUMIZI YA RUZUKU YA MIRADI YA MAENDELEO	YA	13,141,261,532		1,103,843,449	8.4
	JUMLA		127,000,210,329		45,149,616,414	35.6

**1.3 MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA
2021/2022, HADI KUFIKIA DESEMBA 2021.**

- Halmashauri imekusanya jumla ya Shilingi **25,699,533,045** kwa kipindi cha miezi sita Julai 2021 hadi Disemba 2021 ambayo ni sawa na asilimia **51.3** ya malengo ya Mwaka mzima 2021/2022.
- Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2020, jumla ya shiling **13,811,306,421.00** ambayo ni fedha za mapato ya ndani zimetumika

kutekeleza miradi ya kimkakati, upimaji ardhi, malipo ya fidia ya ardhi na miradi ya kijamii.

- Halmashauri imefanikiwa kufungua zahanati mpya ya Makutupora ambayo imeanza kutoa huduma mwezi Novemba, 2021.
- Ujenzi wa mahakama ya Jiji
- Ujenzi wa uzio eneo la Bustani ya Medeli.
- Ununuzi wa magari 3 kwa ajili ya Idara ya Fedha.
- Ununuzi wa vifaa vya upimaji ardhi kwa gharama ya shilingi **240,000,000.00**.
- Katika kipindi cha Julai hadi Disemba Halmashauri imefanikiwa kusajili jumla ya vikundi 371 ambapo vikundi vya wanawake 130, vijana 133, Mchanganyiko 70 na vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha 38.
- Halmashauri imefanikiwa kutoa mikopo kwa vikundi 49, yenyе thamani ya Shilingi **1,039,050,000.00**. Kati ya vikundi hivyo vikundi 19 vya wanawake vimekopa shilingi **524,000,000.00**. Vikundi 19 vya vijana vimekopa shilingi **463,350,000.00** na vikundi 10 vya watu wenye ulemavu vimekopa shilingi **51,700,000.00**.
- Halmashauri imefanikiwa kufanya ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na Watu wenye ulemavu katika Kata **41** katika vikundi 1,489 ambapo jumla ya Tshs **689,922,075.00** zimerejeshwa. Ufuatiliaji bado unaendelea.
- Halmashauri imefanikiwa kutoa mafunzo kwa vikundi vilivyopata mkopo 49 vyenye jumla ya viongozi wa vikundi 147. Mafunzo yalihu Usimamizi wa fedha, Usimamizi wa mradi wa kikundi, Mpango wa biashara, Uongozi na usimamizi wa vikundi, Utunzaji wa kumbukumbu, Ujazaji wa mikataba na Marejesho.
- Halmashauri imefanikiwa kuzifikia Kata zote 41 za Jiji la Dodoma kutoa elimu na kuhamasisha mambo mbalimbali katika jamii yanayohusu:- Mikopo

midogomidogo na upatikanaji wake, UKIMWI, Wanawake na Vijana, Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF), Ukatili wa Wanawake na watoto, na kusimamia Ugawaji wa Fedha za TASAF na Usafi wa Mazingira.

- Serikali kupitia mpango wa kunusuru kaya masikini TASAF kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2021 imewezesha takribani kaya masikini 5,361 kiuchumi kwa kutoa jumla ya shilingi **137,752,000** ambapo baadhi yao wameweza kuanzisha biashara ndogo ndogo, kupata huduma za Afya, Elimu juu ya lishe bora na kusomesha watoto wao. Utekelezaji wa miradi 61 ya kutoa ajira ya muda katika mitaa 77 iliyopo kwenye mpango unaoendelea.
- Ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji wa zabibu Gawaye ambapo miundombinu chakavu imeondolewa na kuweka miundombinu mipyä katika eneo la ekari 45 zimekarabatiwa.
- Ununuzi na usambazaji wa mbegu bora za alizeti zinazostahimili ukame kiasi cha tani 3.
- Uzalishaji wa miche bora ya zabibu ambayo itagawiwa kwa wakulima. Miche hii inazalishwa katika shamba la msalato na Nanenane ambapo miche 152,000 ipo kwenye vitalu hivyo. Hadi sasa kiasi cha miche 3,334 kimeshawafikia wakulima wanaolima zabibu eneo la mpunguzi.
- Utoaji wa mafunzo kwa wataalam 24 na wakulima 450 juu ya njia bora za uzalishaji wa miche, njia bora ya uzalishaji wa zabibu na usindikaji wa zabibu.
- Mwaka 2020/21 Jiji lilipanga kutoa leseni za biashara **10,000** ambapo kuanzia Julai hadi Disemba imefanikiwa kutoa leseni **5,713** sawa na asilimia **57.13**
- Kuendeleza ujenzi wa miradi ya kimkakati ya Dodoma City Hoteli na Government City Complex. Ambapo katika mradi wa hoteli hadi kufikia Disemba 2021, Kiasi cha shilingi **8,907,357,286.24** kimekwisha lipwa kwa fedha za mapato ya ndani sawa na asilimia **89.1** ya shilingi **9,995,881,126.75** zinazohitajika. Ujenzi umekamilika.
- Mradi wa Kitega Uchumi Mtumba unatekelezwa kwa awamu mbili kwa kutumia fedha za mapato ya ndani ambapo kwa awamu ya kwanza hadi kufikia Disemba

2021, kiasi cha shilingi **12,189,688,381.46** kimekwishalipwa sawa na asilimia 64.5 ya Shillingi **18,875,665,009.83** zinazohitajika. Jengo lipo asilimia 90 ya utekelezaji.

- Halmashauri imefanikiwa kufanya uthamini katika maeneo ya Nala, Kikombo, Mtumba na Ihumwa ambapo kiasi cha shilingi **1,328,602,144.35** kimelipwa fidia kwa wananchi kupitia fedha za mapato ya ndani.
- Mwaka 2020/21 Jumla ya viwanja **10,339** vimepimwa katika maeneo ya Ngh'ongh'onha, Hombolo Bwawani, Nala, Zuzu na Mpunguzi.
- Jiji limefanikiwa kuandaa mipango **41** ya matumizi bora ya ardhi.
- Jumla ya hati **8,247** zimetolewa kwa wamiliki mbalimbali kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2020/21.
- Kusimamia Ujenzi wa madarasa 143 ya Shule za Sekondari na 4 ya Shule za Msingi shikizi ya UVICO ambapo kiasi cha shilingi 2,940,000,000.00 zimetumika.
- Kuongezeka kwa ufaulu wa mtihani wa kumaliza elimu ya msingi PSLE 2021 kutoka Asilimia 82 mwaka 2020 hadi kufikia Asilimia 89.9
- Kukamilika kwa ujenzi wa vyumba vyatya madarasa 43 ambapo vyumba 39 vimejengwa kwa mapato ya ndani na vyumba 4 kwa fedha za UVICO

1.4 CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2021/2022.

- Kuongezeka kwa gharama za vifaa vya ujenzi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.
- Mwitikio mdogo wa jamii kwenye uchangiaji wa miradi ya maendeleo.
- Uharibifu mkubwa wa Maliasili na uvamizi wa maeneo yanayotarajiwa kupimwa unaotokana na shughuli za kibinadamu kama kilimo ndani ya hisadhi za Misitu na Uchukuaji wa Madini Ujenzi ndani ya mashamba.
- Kukosa fedha za ruzuku kwa ajili ya uendelezaji wa Makao Makuu inayolazimu Halmashauri kutumia fedha zake za makusanyo ya ndani ambazo hazitoshi.

1.5 MIKAKATI YA KUTATUA CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA MWAKA WA FEDHA 2022/2021.

- Kushirikisha Wadau mbalimbali katika kuchangia maendeleo na kuhamasisha wananchi kuchangia nguvu zao katika kutekeleza miradi ya maendeleo.
- Kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kutunza maliasili na kusimamia sheria za maliasili kwa kuwakamata wanaoharibu.
- Kuhimiza wananchi wanufaika wa miradi kuchangia miradi hiyo.
- Kuomba fedha za maombi maalumu kutoka Serikali Kuu.

2.0 MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

2.1 MAKISIO YA MAPATO YA FEDHA ZA RUZUKU NA MAPATO YA NDANI.

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa mwaka 2022/23 imekadiria kukusanya Mapato yenyeye jumla ya Shilingi **100,948,636,643.00** katika Vyanzo vyake vya ndani, Serikali kuu, Wahisani mbali mbali kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbali mbali za Maendeleo, Utoaji huduma na kujiendesha. Bajeti hii imepungua kw asilimia **20.1** ukilinganisha na bajeti yam waka wa fedha 2021/22. Mchanganuo wa makisio hayo yameainishwa kwenye jedwali lifuatalo: -

SURA YA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2022/23

NA	CHANZO CHA MATUMIZI	MAKISIO YA MWAKA 2021/22 (TZS)
1.	MATUMIZI YATOKANAYO NA MAPATO YA NDANI (Matumizi ya kawaida na Mishahara na vyanzo lindwa)	10,417,319,179.00
2.	MATUMIZI YATOKANAYO NA MAPATO YA NDANI (Miradi ya maendeleo)	19,229,735,962.00
	JUMLA MAPATO YA NDANI	29,647,055,141.00
3.	MATUMIZI YA RUZUKU YA MISHAHARA (PE)	60,292,706,532.00
4.	RUZUKU YA MATUMIZI MENGINEYO (OC)	289,777,000.00
5.	MATUMIZI YA RUZUKU YA MIRADI YA MAENDELEO	10,719,097,970
	JUMLA	100,948,636,643.00

Sababu zilizo sababisha kushuka kwa bajeti ni mabadiliko ya makisio ya mapato ya ndani yaliyo pungua kutoka shilingi **50,116,465,099.00** kwa mwaka 2021/22 hadi shilingi **29,647,055,141.00** kwa mwaka wa fedha 2022/23 ambayo ni sawa na asilimia **41**. Zifuatazo ni sababau zilizosababisha kushuka kwa bajeti ya mapato ya ndani na baadhi ya vyanzo vya fedha:-

- Zoezi la upimaji shirikishi wa viwanja ambao ulitoa asilimia 70 ya mgawanyo wa viwanja kwa Wananchi na hivyo kusababisha wananchi kuwa na viwanja vingi kuliko mamlaka ya upangaji. Hali hii imesababisha kupungua kwa idadi ya viwanja vya Halmashauri na soko la viwanja, hivyo kupungua kwa makisio ya fedha yanayotokana na ardh.
- Kutofikiwa kwa makisio ya mapato ya miradi mikubwa kutokana na miradi hiyo kutofanya kazi kama ilivyokusudiwa baada ya kuitia uhalisia wa vyanzo hivyo wakati wa utekelezaji.
- Tatizo la kuchelewa kupata wawekezaji wa miradi mikubwa.
- Baadhi ya Wafadhili kutotoa ukomo wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/23 wakiwemo UNICEF, Global Fund, NTD, NSP na DFID.

2.2 MUHTASARI WA MAKISIO YA MAPATO YOTE KWA MWAKA 2022/2023

I. MAPATO YA NDANI

	CHANZO	MAKISIO 2021/2022	MAKUSANYO HALISI HADI DISEMBA 30, 2021	MAKISIO 2022/2023
	500A - IDARA YA UTAWALA			
14220129	Mauzo ya Vitambulisho	2,405,000	1,625,000	2,405,000
114450104	Ukumbi wa jiji	14,400,000	4,250,000	14,400,000
	Jumla Ndogo	16,805,000	5,875,000	16,805,000
	500A-KITENGO CHA MANUNUZI			
11450104	Kodi ya pango la nyumba	1,055,262,000	514,489,005	1,055,262,000
14220194	Ada ya Mikataba			

		20,000,000	7,025,000	25,490,000
	Jumla Ndogo	1,075,262,000	521,514,006	1,080,752,000
	5000- KITENGO CHA SHERIA			
14220139	Faini za Ukiukwaji wa sheria	20,000,000	27,181,000	21,000,000
	Jumla Ndogo	20,000,000	27,181,000	21,000,000
	5000 - IDARA YA FEDHA			
11440113	Ushuru wa Huduma	1,815,941,397	1,218,485,098	2,036,768,809
	Jumla Ndogo	1,815,941,397	1,218,485,098	2,036,768,809
	501A -IDARA YA USAFI NA MAZINGIRA			
140894	Ada ya Vyoo vinavyomilikiwa na Jiji	52,925,000	36,600,152	52,925,000
14220190	Ada ya Uzoaji Taka/Kukodi Container	1,200,000,000	596,987,750	1,056,000,000
14210118	Ada ya usajili wa magari ya kunyonya maji taka	450,000	450,000	450,000
11610123	Ada ya Usajili wa Kampuni ya Usafi	250,000	250,000	250,000
11450101	Kibali cha kutumia maeneo ya wazi (Nyerere square na mashujaa)	12,600,000	9,410,000	12,600,000
11610143	Ushuru wa Madini Ujenzi (Mchanga,Kokoti na mawe)	492,750,000	237,026,815	438,000,000
14220194	Faini za Uharibifu wa Mazingira	36,500,000	13,140,000	36,500,000
11610143	Ada ya Vibali vya Madini Ujenzi	1,000,000	1,000,000	1,000,000
14220127	Ada ya ukaguzi wa Mazingira	1,000,000	1,000,000	1,000,000
	Jumla Ndogo	1,797,475,000	895,864,717	1,598,725,000
	502E - KITENGO CHA BIASHARA NA MASOKO			
11451111	Ada ya Usajili wa vyombo vya moto	63,385,000	39,728,100	77,806,500

14210122	Huduma ya Maji Soko kuu la Majengo	1,200,000	900,000	1,200,000
11610140	Ada ya maombi ya leseni za biashara na vileo	97,520,000	36,522,800	80,000,000
11610103	Ada ya kuhamisha leseni	220,000	160,000	220,000
11610127	Upotevu wa leseni za biashara (Utoaji nakala ya leseni)	240,000	220,000	240,000
14220194	Faini za kisheria za biashara	15,000,000	12,550,000	15,000,000
11610103	leseni za Biashara	1,705,000,000	1,009,611,710	1,800,000,000
11310103	Ushuru wa Nyumba za Kulala wageni	497,700,000	330,830,949	600,000,000
142200162	Pango la vibanda vya soko kwa masoko yote	268,320,000	122,149,000	224,712,000
	Jumla Ndogo	2,648,585,000	1,552,672,559	2,819,458,500
IDARA YA ELIMU MSINGI - UTAMADUNI				
11610111	Ada ya Burudani na kumbi za starehe	69,600,000	37,396,000	70,000,000
	Jumla Ndogo	69,600,000	37,396,000	70,000,000
DODOMA JIJI FC				
	Mauzo ya Tiketi / Viingilio		595,403,634	
	Jumla Ndogo		595,403,634	
IDARA YA AFYA				
14230104	CHF	208,255,500	26,194,976	120,000,000
14230104	NHIF	303,941,800	29,808,653	300,000,000
14230104	User fee	694,560,000	322,664,609	690,000,000
12110104	Ada ya ukaguzi wa majengo ya Biashara	70,000,000	17,678,500	50,000,000

	Ada ya Upimaji afya	20,000,000	10,060,000	20,000,000
	Jumla ya Ndogo	1,296,757,300	409,783,738	1,180,000,000
505 - USHURU WA MIFUGO NA UVUVI				
14220175	Ushuru wa Masoko ya Mifugo (Minada)	96,156,000	70,459,650	110,000,000
	Ada ya Chanjo za mifugo	45,000,000	41,299,230	25,000,000
14220176	Ushuru wa Machinjio na Ukaguzi	69,408,000	44,824,036	85,320,000
14220191	Leseni za Uvubi na ushuru wa samaki	7,470,000	2,917,000	7,420,000
	Jumla Ndogo	218,034,000	159,499,916	227,740,000
506A - IDARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA				
142101125	Ushuru wa Mazao	89,572,602	91,466,300	120,000,000
	Jumla Ndogo	89,572,602	91,466,300	120,000,000
511A - IDARA YA UJENZI				
	Ukodishaji Mitambo	20,000,000	22,980,000	-
114451115	Ushuru wa Stendi kuu ya Mabasi/changombe,s abasaba,kikuyu,kizot a	150,000,000	93,089,400	150,000,000
14210116	Ada ya Ukaguzi wa ramani na vibali vya ujenzi	483,000,000	321,549,670	499,200,000
	Jumla Ndogo	653,000,000	437,619,070	649,200,000
512H - KITENGO CHA YA MISITU				
11610144	Ushuru wa Mazao ya Misitu	48,600,000	31,359,500	60,000,000
	Uuzaji wa miche	5,000,000	630,000	5,000,000
	Jumla Ndogo	53,600,000	31,989,500	65,000,000

512A -MIPANGOMIJI, ARDHI NA MALIASILI				
14220146	Ada ya Maombi ya Viwanja	140,000,000	110,300,000	180,000,000
11450101	Ukodishaji maeneo ya Wazi	70,000,000	28,461,078	47,682,480
11460104	Mauzo ya viwanja na Ada ya umilikishaji wa Ramani	32,260,000,000	18,498,414,400	15,000,000,000
11310104	Mapato tokana na Minara	129,400,000	29,200,000	129,400,000
	Ada ya kubadili matumizi	5,520,000	-	5,520,000
	Tozo ya Ujenzi	-	-	84,000,000
	Ada ya maandalizi ya Michoro ya Mipangomiji			36,000,000
	Jumla Ndogo	32,604,920,000	18,719,375,478	15,482,602,480
KITENGO CHA NYUKI				
14210135	Ada ya Mazao ya Nyuki	10,000,000	8,807,400	12,000,000
	Jumla Ndogo	10,000,000	8,807,400	12,000,000
IDARA YA MAENDELEO YA JAMII				
11450104	Mapato yatokanayo na vibanda, vyumba na ukodishaji ukumbi eneo la Community centre	106,908,000	51,928,000	106,908,000
	Usajili wa vikundi	13,080,000	7,853,000	5,520,000
	Ada ya Usajili wa NGO's	-	-	2,400,000
	Jumla Ndogo	119,988,000	59,781,000	114,828,000
IDARA YA ELIMU - SEKONDARI				
14220196	Ada za wanafunzi wa kidatu cha tano	354,820,000	260,720,500	354,820,000

	na Sita			
	Jumla ndogo	354,820,000	260,720,500	354,820,000

IDARA YA MIPANGO TAKWIMU NA UFUATILIAJI				
	Mauzo ya Tofali - LOW COST (FAIDA)	1,501,000,000	176,765,660	799,984,800
	Council Investment Complex	-		784,990,552
	Stendi kuu	1,316,878,800	365,290,364	827,350,000
	Soko kuu	2,576,976,000	84,191,206	463,620,000
	Lory Park	821,250,000	20,250,900	205,410,000
	Chinangali park	216,000,000	22,600,000	216,000,000
	City hotel	840,000,000	-	500,000,000
	Jumla ndogo	5,771,104,800	669,098,130	3,797,355,352
	JUMLA KUU MAPATO YA NDANI	50,116,465,099	25,699,533,045	29,647,055,141

RUZUKU YA MISHAHARA NA MATUMIZI MENGINE

KIFUNGU	CHANZO	MAKISIO 2021/2022	MAPATO JULAI HADI DISEMBA 2021	MAKISIO 2022/23
500A - UTAWALA				
13310101	Mishahara	8,364,959,174	2,587,881,421	3,197,850,300
13310102	Matumizi Mengine (Utawala)		381,119,824	
	Jumla Ndogo 500A	8,364,959,174	2,969,001,245	3,197,850,300
505A MIFUGO NA UVUVI-UTAWALA				
13310101	Mishahara	1,071,491,280	274,072,000	700,620,000
13310103	Matumizi mengine (Oc)		4,230,665	12,692,000
	Jumla Ndogo 505A	1,071,491,280	278,302,665	713,312,000

506A - KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA - UTAWALA				
13310101	Mishahara	888,678,970	219,994,000	382,420,000
13310103	Matumizi mengine (Oc)	24,730,000	5,015,834	12,038,000
	Jumla Ndogo 506A	913,408,970	225,009,834	394,458,000

507A - ELIMU MSINGI				
13310101	Mishahara	27,355,993,216	10,503,900,300	25,545,846,000
13310104	Matumizi mengine (Oc)	64,486,000	5,373,833	64,286,000
13310105	Likizo	231,140,000	115,750,000	231,140,000
13310106	Uhamisho	201,538,000	136,100,000	173,000,000
	Jumla Ndogo 507A	27,651,619,216	10,761,124,133	26,014,272,000

508A TIMU YA MENEJIMENTI YA AFYA YA HALMASHAURI				
13310101	Mishahara	9,113,451,248	2,963,688,000	6,638,250,660
13310105	Matumizi mengine (Oc)	133,634,000	64,678,304	133,634,000
	MSD Transer	593,897,200		
	On call alowance	62,829,000	26,178,750	62,829,000
	Jumla Ndogo 508A	9,903,811,448	3,054,545,054	6,834,713,660

509A - ELIMU SEKONDARI - UTAWALA				
13310101	Mishahara	14,989,498,286	8,920,023,500	20,914,356,000
	Likizo	43,698,000	96,600,000	72,076,000
13310104	Matumizi mengine (Oc)	43,698,000		40,160,000
	Jumla Ndogo 509A	15,076,894,286	9,020,265,000	21,026,592,000

511A UJENZI UTAWALA				
13310104	Mishahara	536,132,323	195,606,000	313,518,000
13310105	Matumizi mengine (Oc)	22,629,000	9,428,750	22,629,000

	Jumla Ndogo	558,761,323	205,034,750	336,147,000
MISHAHARA IDARA MBALIMBALI		2,382,158,041.	952,863,216.40	1,904,699,572
Jumla - Mapokezi ya fedha za mishahara		62,320,204,497	25,665,165,221	60,292,706,532.
Jumla - Mapokezi ya fedha za Matumizi Mengineyo		1,422,279,200	848,117,460	285,439,000
Jumla - Ruzuku ya Mishahara na Matumizi Mengineyo		63,742,483,697	26,513,282,681	60,707,483,532

MIRADI YA MAENDELEO SERIKALI KUU NA WAHISANI

KIFUNGU	CHANZO	MAKISIO 2020/2021	MAPATO JULAI HADI DESEMBA 2021	MAKISIO 2022/23
508A - AFYA (CHMT)				
13110103	Global Fund	19,943,505	-	
13120122	Other Sources (VACCINE DELIVERY SUPPORT)	599,999,949	34,672,970	
13110105	UNICEF	10,000,000	-	
	Special Fund	586,766,772	850,000,000	
	DFID	37,000,000	-	
	NSP	24,000,000	-	
	NTD	15,549,000	-	
	Health Sector Busket Fund (HSBF)	853,595,400	166,642,917	853,595,469.52
	Jumla ya Ndogo 508A	2,146,854,626	1,051,315,887	853,595,469.52
509B - ELIMU MSINGI				
	EQUIP FUND	336,600,000	-	
	School meal	129,276,000	353,061,647	129,276,000

	Other Sources (COVID-19 MADARASA SHULE SHIKIZI)	123,125,000	80,000,000	
	P4R	346,581,500	76,493,522	346,581,500
	Responsibility Allowance	336,600,000		336,600,000
	Central Government Grant	125,000,000		125,000,000
	Examination grant	455,670,009		455,670,009
	Ruzuku ya Capitation	454,620,000		607,284,000
	Jumla ya Ndogo 508A	935,582,500	509,555,169	1,653,830,009.00
509B - ELIMU SEKONDARI				
	Examination Grant	1,057,239,000	784,718,020	601,964,500
	Capitation Grant	917,634,000	98,514,522	310,343,818.80
130103	Responsibility Grant	117,000,000	68,250,000	117,000,000
	School Fees compasation	508,880,000	414,598,038	508,880,000
	School meal	1,116,180,000		1,116,180,000
	Other Sources (COVID-19 MADARASA SHULE SHIKIZI)	292,519,172	2,860,000,000	
	P4R	346,581,500	98,924,922	200,000,000
	Quality aiampromvement (SEQUIP)	1,909,382,734	470,000,000	198,940,000
	Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo kutoka Serikali Kuu	639,098,672.41		639,098,672.41
	Jumla ya Ndogo 509B	6,265,416,406	4,795,005,502	3,692,406,991.21
503B-MFUKO WA JIMBO				
13320107	Mfuko wa kuchocheara maendeleo	70,484,000	70,484,000	70,484,000
	Jumla ya Ndogo 503B	70,484,000	70,484,000	70,484,000

**504B - MAENDELEO YA JAMII
JINSIA NA WATOTO**

130121	TASAF-NVF	3,722,924,000	423,959,120	3,722,924,000
	Jumla ya Ndogo 504B	3,722,924,000	423,959,120	3,722,924,000
	Jumla Miradi ya Maendeleo	13,141,261,532	6,426,360,558	10,719,097,970
	JUMLA KUU	127,000,210,329	58,639,176,284	100,948,636,643

3.0 MIKAKATI YA KUKUSANYA MAPATO KWA MWAKA 2022/23

- Kuwatumia Watendaji wa Kata na Mitaa ili waweze kukusanya mapato katika maeneo yao.
- Kuendelea kukusanya na kufanya uchambuzi “assessment” wa vyanzo vya mapato vya Halmshauri ili kukusanya takwimu sahihi za vyanzo vya mapato.
- Kuhakikisha ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo na vituo vyote unatumia mfumo wa kielectroniki ili kuweza kudhibiti upotevu wa mapato.
- Kuandaa kanzi data ya viwanja vyote vinavyozalishwa ili kudhibiti utoaji/ulipaji na uendelezaji.
- Kuandaa mfumo wa ufuatilaji wa majalada yote ya Halmashauri ikiwemo yanayohusu mapato.
- Kufanya tathmini ya madeni ambayo Halmashauri inadai ili kuongeza mapato.
- Kuanzishwa kwa Kampuni (SPV) itakayo simamia miradi yote ya Kimkakati (Dodoma City Hotel, Council Investment Complex, Low-Cost Housing, Soko Kuu la Job Ndugai, Kituo Kikuu cha Mabasi na Nala Lorry Park)

Nawasilisha



Joseph C. Mafuru
Mkurugenzi wa Jiji,
DODOMA.

23

MATUMIZI MENGINEYO
RUZUKU(OC)

IDARA YA AFYA

MPANGO NA BAJETI YA MATUMIZI MENGINEYO RUZUKU (OC) KWA MWAKA 2022/23

KASMA (Vote Number) 508A
NAMBA YA LENGO

JINA LA KASMA (Vote Name)
MAELZO YA LENGO

LENGO C KUBORESHA UPATIKANAJI NA UTOAJI WA HUDUMA BORA ZA JAMII KWA USAWA

1 SHABAHA **Uhaba wa watumishi wa Afya wenye Ujuzi umepungua kutoka 39% hadi 10% kufikia Juni**

NA	Shughuli	Kasma	Maelezo	Kipimo (Unit)	Idadi (Qu)	Gharama	Makisio
1	Kufanya usambazaji wa chanjo kutoka stoo ya wilaya kwenda kwenye vituo 35 vya kutolea huduma za afya ifikapo Juni 2023	22003102	Dizeli	Lita	1840	2,500.00	4,600,000
		21211105	Posho ya kulalanje ya kituo	Kila Mmoja	60	50,000.00	3,000,000
							7,600,000
2	Kutoa Stahiki za kisheria kwa watumishi 120 wanaotoa huduma za afya kufikia Juni 2023	21113117	Nauli ya likizo	Kwa jumla (Lampsum)	34	300,000.00	10,200,000.00
		21113129	Mizigo	Kila mmoja	1	2,497,500.00	2,497,500.00
		22032111	Mazishi	Kila mmoja	4	540,000	2,160,000.00
JUMLA NDOGO							14,857,500.00
3	Kutoa stahiki kwa Mkuu wa idara kila mwezi hadi kufikia Juni 2023	21113122	Nyumba	Mtu	6	600,000.00	3,600,000.00
			Umeme	Mtu	6	210,000.00	1,260,000.00
		21121101	Simu	Mtu	6	180,000.00	1,080,000.00

NA	Shughuli	Kasma	Maelezo	Kipimo (Unit)	Idadi (Qu)	Gharama	Makisio
JUMLA NDOGO							5,940,000.00
4	Kufanya vikao 4 vya kisheria vya bodi ya afya kila robo na kikao 1 cha bajeti ifikapo Juni 2023	21113103	Posho ya kikao (Sitting allowance)	Watu	5	2,050,000.00	10,250,000.00
		21113103	Huduma ya chakula	wajumbe	70	12,000.00	840,000.00
JUMLA NDOGO							11,090,000.00
5	Kutoa zawadi kwa mtumishi anaefanya vizuri siku ya wafanyakazi ifikapo Juni 2023	2202021	Zawadi	Watu	2	500,000.00	1,000,000.00
JUMLA NDOGO							1,000,000.00
6	Kuwezesha upatikanaji wa viburudisho ofisi ya mganga mkuu ifikapo Juni 2023	21121103	Viburudisho	Watu	108	20,000.00	2,160,000.00
JUMLA NDOGO							2,160,000.00
7	Kuwezesha uaandaaji wa taarifa za LAAC za mwaka 2021/2022 ifikapo Juni 2023	22010105	Posho ya kulala nje ya kituo	Watu	50	50,000.00	2,500,000.00
JUMLA NDOGO							2,500,000.00
8	Kuwezesha uandaaji wa bajeti ya mishahara ya watumushi wa Idara ya Afya kwa mwaka 2023/2024 ifikapo	22010105	Posho ya kulala nje ya kituo	Watu	28	60,000.00	1,680,000.00
JUMLA NDOGO							1,680,000.00

Nguuli	Kasma	Maelezo	Kipimo (Unit)	Idadi (Qu)	Gharama	Makisio
9 Kufanya matengenezo ya magari 3 kwaajili ya ofisi ya mganga mkuu kwaajili ya usimamizi shirikishi ifikapo juni 2023.	22024106	Matengenezo	kila moja	4	500,000.00	2,000,000.00
JUMLA NDOGO						2,000,000.00
10 Kufanya usimamizi shirikishi kwenye vituo 104 vya kutolea huduma za afya ifikapo Juni 2023	22003102	Dizeli	Lita	2000	2500	5,000,000.00
JUMLA NDOGO						5,000,000.00
11 kufanya matengenezo kinga ya kompyuta 10 na kiyoyozi 1 kila robo ifikapo Juni 2023	22024106	Matengenezo	lumpsum	1	500,000	500,000.00
JUMLA NDOGO						500,000.00
12 Kuwezesha ununuzi wa kompyuta Mpakato 4 kwa ajili ya matumizi ya ofisi kila robo mwaka ifakapo Juni 2023		Kompyuta	Seti	4	2500000	10,000,000.00
JUMLA NDOGO						10,000,000.00

NA	Shughuli	Kasma	Maelezo	Kipimo (Unit)	Idadi (Qu)	Gharama	Makisio
13	Kuwawezesha wajumbe 3 wa timu ya uendeshaji wa huduma za Afya (CHMT) kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi kila robo mwaka ifikapo Juni 2023	22008105	Ada	Watu	5	500,000.00	2,500,000.00
		22010102	Nauli	Watu	5	20,000.00	100,000.00
		22010105	Posho ya kulala nje ya kituo	Watu	25	100000	2,500,000.00
Jumla ndogo							5,100,000.00
14	Kununua samani (viti4, meza 4 na kiti kimoja cha wateja) katika ofisi ya Mganga Mkuu ifikapo Juni 2023.	31122211	Samani	lumpsum	1	5,000,000.00	5,000,000.0
JUMLA NDOGO							5,000,000.0
15	Kuwezesha upatikanaji wa shajala Seti 4 kwa kila robo mwaka ifakapo Juni 2023		Shajala	Seti	4	1,044,225.00	4,176,900.0
JUMLA NDOGO							4,176,900.0
JUMLA OFISI YA MGANGA MKUU							78,604,400.00

NA	Shughuli	Kasma	Maelezo	Kipimo (Unit)	Idadi (Qu)	Gharama	Makisio
----	----------	-------	---------	---------------	------------	---------	---------

VOTE: 5012

(Vote name)....VITUO VYA AFYA

NA	SHUGHULI ZILIZOPANGWA		MAELEZO	KIPIMO	IDADI	GHARAMA	MAKISIO
16	Kutoa Stahiki za kisheri kwa watumishi wapatao 20 katika zahanati hadiu Juni 2023.	21113129	Mizigo	kila mmoja	8	500,000.00	4,000,000.00
		22032111	Mazishi	kila mmoja	8	540,000.00	4,320,000.00
		21211105	Posho ya kulala nje ya kituo	kila mmoja	20	100,000.00	2,000,000.00
		21110225	sare	kila mmoja	30	120,000	3,600,000.00
		21113119	Matibabu	kila mmoja	4	781,200.00	3,124,800.00
		21113117	likizo	kila mmoja	15	500,000.00	7,500,000.00
		21113115	Posho ya watumishi wa ajira mpya	lumpsum	8	700,000.00	5,600,000.00
JUMLA NDOGO VITUO VYA AFYA						30,144,800.00	

VOTE: 5013

(Vote name)....ZAHANATI

NA	SHUGHULI ZILIZOPANGWA		MAELEZO	KIPIMO	IDADI	GHARAMA	MAKISIO	
17	Kutoa Stahiki za kisheri kwa watumishi wapatao 20 katika zahanati hadiu Juni 2023.	21113129	Mizigo	kila mmoja	4	500,000.00	2,000,000.00	
		22032111	Mazishi	kila mmoja	4	540,000.00	2,160,000.00	
		21211105	Posho ya kulala nje ya kituo	kila mmoja	20	100,000.00	2,000,000.00	
		21110225	sare	kila mmoja	15	120,000	1,800,000.00	
		21113119	Matibabu	kila mmoja	4	781,200.00	3,124,800.00	
		21113117	likizo	kila mmoja	15	500,000.00	7,500,000.00	
		21113115	Posho ya watumishi wa ajira mpya	lumpsum	9	700,000.00	6,300,000.00	
JUMLA NDOGO ZAHANATI						24,884,800.00		
JUMLA KUU						133,634,000.00		

MPANGO WA BAJETI YA IDARA YA ELIMU SEKONDARI MWAKA 2022/2023
MATUMIZI YA KAWAIDA - RUZUKU (OC)

LENGO C :		Kuboresha upatikanaji na utoaji wa huduma bora za kijamii na kwa usawa					
NA.	SHABAHA 01	Kuongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wanaomaliza elimumsingi kutoka 74.05% mpaka 95% ifikapo Juni, 2025					
	Shughuli	Kasma	Maelezo	Kipimo	Idadi	Gharama kwa Kipimo	Makisio
1	Kuratibu shughuli za kila siku za ofisi ya Afisa elimu sekondari ifikapo Juni 2023	21113103	Masaa ya ziada	Mtu	220	30,000.00	6,600,000.00
		22003102	Mafuta ya gari (Diesel) lita 2,500	Lita	400.00	2,500.00	1,000,000.00
Jumla Ndogo							7,600,000.00
2	Ufutiliaji na kufanya tathimini ya ufundishaji na ujifunzaji wa mara kwa mara kwa shule 58 za sekondari ifikapo Juni, 2023	22003102	Mafuta ya gari (Diesel) lita 2,500	Lita	1200	2,500.00	3,000,000.00
		22010105	Posho ya kujikimu	mtu	50	120,000.00	6,000,000.00
		22014104	viburudisho	mtu	150	10,000.00	1,500,000.00
		22021107	Matengenezo ya gari	bili	2	1,000,000.00	2,000,000.00
Jumla Ndogo							12,500,000.00

SHABAHA 02		Kuboresha ufaulu wa wanafunzi na kuweka mazingira rafiki kwa watumishi wa Idara,wakuu wa shule na walimu ifikapo Juni, 2025						
NA.	Shughuli	Kasma	Maelezo	Kipimo	Idadi	Gharama kwa Kipimo	Makisio	
4	Kuboresha mazingira rafiki kwa watumishi wa idara ya elimu sekondari ifikapo Juni, 2023	21113119	Matibabu	mtu	2	500,000.00	1,000,000.00	
			Kujikimu ajira Mpya	mtu	8	700,000.00	5,600,000.00	
		22008108	vifaa vya mafunzo	seti	4	400,000.00	1,600,000.00	
		22032111	Gharama za mazishi	Mtu	2	1,000,000.00	2,000,000.00	
		Jumla Ndogo					10,200,000.00	
5	Kubaini vipaji mbalimbali vya wanafunzi katika michezo katika shule 58 za sekondari ifikapo Juni, 2025	22021107	Ununuizi wa taili na batri	Bill	2	500,000.00	1,000,000.00	
		21121107	Ununuizi wa vifaa vya ofisi	seti	180	10,000.00	1,800,000.00	
		22032111	Manunuizi ya vifaa vya kompyuta	Seti	2	500,000.00	1,000,000.00	
		21121107	Ununuizi wa samani za ofisi	Seti	3	500,000.00	1,500,000.00	
		Jumla Ndogo					5,300,000.00	
SHABAHA 03		Kubaini vipaji mbalimbali vya wanafunzi katika michezo katika shule 58 za sekondari ifikapo Juni, 2025						
NA.	Shughuli	Kasma	Maelezo	Kipimo	Idadi	Gharama kwa Kipimo	Makisio	
6	Kuboresha na kusimamia michezo katika shule za sekondari (UMISSETA) Ifikapo Juni, 2023	22010105	Posho ya kujikimu	Mtu	10	120,000.00	1,200,000.00	
		22003102	Mafuta ya gari (Diesel)	Lita	944	2,500.00	2,360,000.00	
		22014106	Kutoa zawadi kwa washindi 20	mtu	20	50,000.00	1,000,000.00	
Jumla ndogo						4,560,000.00		
Jumla kuu						40,160,000.00		

IDARA YA ELIMU MSINGI

BAJETI YA MATUMIZI MENGINE (OC) KWA FEDHA ZA RUZUKU YA KUTOKA SERIKALI KUU MWAKA 2022/2023
KASMA 5007 JINA LA KASMA

NAMBA YA LENGO : C

MAELEZO YA LENGO Kuboresha upatikanaji wa huduma za jamii kwa usawa

Na	Shughuli	Maelezo	GFS CODE	Kipimo	Kiasi	Gharama	Makisio
SHABAHA 1 : Mazingira ya kazi kwa maafisa wa elimu 16, dereva 1, wahudumu wa ofisi 3, dereva 1, mhasibu 1 na PS 1 kuboreshwa ifikapo Juni 2023							
1	Kufanya usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za ufundishaji na ujifunzaji katika shule 148 ifikapo June 2023	Diesel	22003102	3258.4	2,500.00	8,146,000.00	
	[22001101] Office Consumables (papers,pencils, pens and stationaries)	Set		1	5	500,000.00	2,500,000.00
	Posho ya kazi kwa saa za ziada	21113103	Posho	639	30,000.00	19,170,000.00	
	Chakula na viburudisho	22014104	Mtu	442	10,000,000.00	4,220,000.00	
2	Kuwezesha upatikanaji wa stahiki za walimu 1000 na maafisa elimu 15 ifikapo Juni 2025	Gharama za matibabu	21113119	Mtu	7	500,000.00	3,500,000.00
		Gharama za mazishi	22032111	Mtu	9	750,000.00	6,750,000.00
		Posho ya kujikimun-dani	22010105	Mtu	200	100,000.00	20,000,000.00
		Jumla ndogo					64,286,000.00

IDARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA

BAJETI YA MATUMIZI MENGINEYO RUZUKU (OC) 2022/2023

NAMBA YA LENGO: C

**MAELEZO YA LENGO : Kuboresha
upatikanaji na utoaji wa huduma bora za
kijamii.**

NA	SHUGHULI	KASMA	MAELEZO	KIPIMO	KIASI	GHARAMA	MAKISIO	
SHABAHA:1 Kuboresha mazingira ya utendaji Kazi kwa watumishi 25 wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika kwa kutoa stahiki za kisheria za watumishi na vitendea kazi ifikapo Juni,2026								
1	Kuwezesha kutoa motisha, stahiki za kisheria za watumishi ifikapo June, 2023	21113101	Likizo	kila moja	2	350,000	700,000	
		22032111	Gharama za mazishi	Kila moja	1	750,000	750,000	
Jumla ndogo							1,450,000	
2	Kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi 30 ifikapo June, 2023	22024101	Matengenezo madogo	Jumla	1	100,000	100,000	
		22006105	Vifaa vya kujikinga	Pic	7	50,000	350,000	
		22001101	Shajara	Kilamoja	40	12,000	480,000	
		21121103	Viburudisho	Robo	4	150,000	600,000	
Jumla ndogo							1,530,000	
SHABAHA : 2 Kutoa mafunzo ya teknolojia mbalimbali za kilimo bora kwa wakulima 6,500 kupitia vishamba vya mfano,maonesho ya kilimo,mashamba darasa na ziara za mafunzo ifikapo Juni,2026								
3	Kutoa mafunzao ya kanuni bora za kilimo na kilimo himilivu kwa wakulima 4,500 na wataalam 25 ifikapo Juni,2023	22021101	Matengenezo ya gari	Kila moja	1	500,000	500,000	
		22001101	Shajala	Kila moja	20	10,000	200,000	
		22003102	Diseli	lita	196	2,500	490,000	
		22001101	Wino/shajala	Kila moja	1	250,000	250,000	
		21113103	Posho ya kujikimu nje ya kituo	Kila moja	23	100,000	2,300,000	
		21113103	Masaa ya ziada	Siku	50	30,000	1,500,000	
		Jumla ndogo					5,240,000	

SHABAHA: 3 Udhibiti wa visumbufu vya mazao na uthibiti ubora wa mbegu za kuazimia ubora (QDS) ifikapo Juni, 2026

